Kabla ya harusi

- Kama utafanya engagement party basi panga siku kabisa
- Utafanya kitchen party au bridal shower? Anza maandalizi
- Siku yako ya Send off
- Unafikiria kufanya nini kwenye fungate? Fikiria maandalizi

Harusi yako

ZINGATIA

Kwa kila malipo unayofanya usisahau kuandikishana au kuchukua stakabadhi (receipt)

- Ni vema kuwa na jalada ambapo utahifadhi habari zako zote kuhusiana na harusi yako
- Fikiria unataka harusi ya aina gani, ndogo watu wa karibu tu, kubwa na ya kifahari, ya kati kati, ukumbi wa nje? Ndani?
- Kuna watu wanatoka mbali watakaohitaji malazi? Fanya mipango sasa
    - Ndugu jamaa na marafiki wanaweza kuwahifadhi?
    - Fanya booking na hoteli au Nyumba za wageni
- Amua unataka kutumia kiasi gani cha pesa na wapi pa kukipata Unaweza kupata msaada hapa
- Chagua siku yako ya harusi, vigezo vyaweza kuwa muda wa watu wenu wa karibu au upatikanaji wa ukumbi au kanisa fulani, angalia kama ni siku ya sikukuu
- Umeshaamua rangi ya harusi yako?
- Umeshachagua wasimamizi wako? Wataarifu na kuwaeleza nini unategemea toka kwao
- Je kuna mila au tamaduni zozote ambazo inabidi kuzitilia maanani? Fanya utafiti. Baadhi ya makabila hufanya hivi
- Andaa ratiba ya harusi
- Usiku wa harusi, fanya booking ya hotel
- Paki kabisa vitu kwaajili ya usiku wa harusi, kama kuna vinavyokosekana fanya mipango ya kununua
- Je utasafiri kwaajili ya fungato? Fanya booking sasa
- Hakikisha una passport, viza, chanjo (kadi ya njano)

SHEREHE

Ukumbi **Maswali ya kuuliza kuhusu ukumbi**

- Anza kufikiria ukumbi, angalia hapa...omba ushauri kwa rafiki ndugu na jamaa
- Chagua ukumbi wa harusi, baadhi iko hapa
- Tembelea kumbi ulizozichagua kwa habari zaidi set a date
- Kama umeona ukumbi unaoupenda katika siku unayotaka, book huo ukumbi
- Fanya malipo ya awali kama umeridhika na mahali hapo, kumbuka kuandikishana au kuchukua stakabadhi halali

Maswali

- Maegesho ya magari
- Idadi ya juu ya watu wanaoweza kuwepo kwa wakati mmoja
- Je wanatoa huduma ya chakula
- Je wanatoa huduma ya vinywaji
- Viti na meza je?

Viti, meza na maturubai

- Kama ukumbi hauji na viti na meza, fanya mipango ya kupata mahali pengine kama hapa
- Kama ni ukumbi wa nje na hali ya hewa inafaa maturubai, inabidi kufanya mpango huo

Chakula na huduma nyingine

- Fikiria unataka kuserve chakula gani
- Tafuta caters na kuwafanyia mahojiano, wengine wako hapa
- Chagua cater kama umeridhika na mkubaliane bei na menu
- Fanya malipo ya awali bila kusahau stakabadhi yako

Vinywaji na wahudumu

- Mpaka sasa unajua ni vinywaji gani unataka na kwa kiasi gani
- Ukumbi unatoa huduma hii ya vinywaji? Je iko ndani ya budget yako?
- Kama la tafuta mtu wa kukuletea vinywaji
- Nani atahudumia, ukumbi unatoa wahudumu? Au mtu wa vinjwaji?
- Fanya makubaliano, toa malipo ya awali
- Usisahau **Champagne**, yenye kilevi au la? Angalia mapendekezo

Keki

- Keki, chagua aina unayotaka na nani atakayekutengenezea, anza na cater wako
- Lipia keki yako

MAVAZI NA UREMBO

Gauni

- Bi Harusi, anza kufikiria nguo yako ya harusi, unataka gauni la aina gani, agalia mifano hapa. Uliza maswali muafaka
- Nguo ya bi harusi, umeshaamua ni aina gani? Au umeiona haswa unayoitaka?
- Kama nguo yako ni ya kununua, nenda kaijaribu, kama ni ya kushona fikiria au pata ushauri juu ya mafundi wa nguo za harusi, unaweza kuanza na hawa
- Gauni la harusi vipi? Kama umepima na umepata unachotaka lipia na chukua, kama ni la kushonesha anza kushona kwa fundi uliyemchagua, mtajie siku ya harusi ambayo ni mwezi mmoja kabla ya harusi

- Kama gauni ni la kukodisha hakikisha umelipeleka kusafishwa dry cleaner
- Anza kutafuta nguo za wasimamizi wako, watanunua au kushona?

Shela and weaving au rasta
- Mara nyingine gauni haliji na shela unayoitaka, anza kutafuta...angalia maduka ya nguo za harusi
- Unafikiria kushonea weaving au kusuka rasta, aina gani na mtindo gani? Angalia mifano hapa

Mapambo mengine
- Hereni, Chain, bangili, viatu, gloves, pochi, vibanio

SALUNI

Nywele na vipodozi
- Nywele, unataka ziwe vipi? Kama utasuka rasta panga siku kabisa na book msusi
- Chagua saluni utakayopambiwa, ni vema kuchagua saluni inayotoa kuhuma zote unazohitaji
- Fanya majaribio ya utakavyobana nywele
- Unaweza kutaka kukata nywele pia, style gani?

Ngozi na kucha
- Fanya miadi ya kutengeneza kucha (pedicure, manicure) na kutengeneza ngozi (facial, waxing
- Ni vema kufanya shughuli hizi mapema kabla ya siku ya harusi

BWANA HARUSI

Suti ya bwana harusi
- Mkumbushe bwana harusi kufuatilia nguo yake na m(wa)simamizi wake

Mapambo ya bwana harusi
- Cuflinks, viatu

KANISANI/MSIKITINI/KAMISHNA
- Andikisha harusi yenu walau mwezi mmoja kabla ya siku
- Kuna semina mbalimbali makanisani na misikitini kwa maharusi watarajiwa, chunguza ni lini na fanya mpango kuhudhuria

MAUA NA MAPAMBO
- Wapambaji angalia baadhi ya mapambo
- Chagua uliyeridhishwa naye na kukubaliana aina ya mapambo na maua
- Usisahau maua ya bibi harusi kama utapenda
- Ingia naye makubaliano na lipia gharama za awali

MC na MUZIKI

- Muziki na msema chochote, angalia hawa, kutana nao kuwaeleza unataka sherehe ya aina gani.
- Wimbo wa kufungulia dansi your wedding song hakikisha MC au bendi ya muziki wanao
- Kama umeshachagua MC, na muziki, book na fanya malipo ya awali, ni vyema kuandikishana

PICHA ZA MNATO NA VIDEO

- Angalia baadhi yao na kazi zao hapa
- Kuna wale ambao wataweka picha zako kwenye album yako ndani ya hii tovuti yako na kuwa rahisi kushirikisha ndugu, jamaa na marafiki.
- Umeridhishwa na mmoja? Panga kuonana naye na kufanya makubaliano

KADI NA MIALIKO

Invitation cards

- Anza kufikiria orodha ya wageni wako wageni wako
- Orodhesha wageni wako, chukua majina toka kwa wazazi wa pande zote mbili na yenu pia
- Kamilisha orodha yako ya wageni, umetumia msaidizi?
- Kuna maneno maalumu unataka kuandika kwenye kadi? Anza kuyaandaa
- Nunua au tengeneza kadi za mwaliko, hawa wanaweza kukusaidia
- Tuma ujumbe kwa watu walioko katika orodha yako kuhusu siku yako ya harusi, ili wasifanye mipango mingine katika siku hiyo (Save this date)
- Tuma kadi za mwaliko walau mwezi mmoja kabla ya harusi
- Andaa ratiba ya harusi na kuiprint, inaweza kuambatana na kadi za mwaliko

Thank you notes/chocolates/ handkerchiefs

PETE

- Anza kutafuta pete unazotaka
- Amua ni pete zipi, zinapatikana duka gani? fanya vipimo
- Nunua pete

USAFIRI

- Tengeneza ratiba ya usafiri na ni magari mangapi na ya aina gani yanatakiwa
- Tafuta usafiri, kama ni wa kukodi ni vyema kuyaona magari. Wanaotoa huduma hii
- Fanya malipo ya awali na kukubaliana mpango wa safari

ZAWADI

- Unataka zawadi gani, chagua zawadi zako ili usipate seti kumi za sahani na vikombe, ziorodheshe hapa

MENGINEYO

- Kama kuna maonesho yoyote maalumu yaandae na kuyaweka katika ratiba
- Usisahau kitabu cha wegeni kama utataka
- Jiandae mapema kwa fungate, nunua vitu utakavyohitaji mapema kabla ya harusi, vipaki kabisa

Kwa kila malipo unayofanya usisahau kuandikishana au kuchukua stakabadhi (receipt)
Mara mahali, saa na utaratibu utakapokua kamili, wasiliana na watoa huduma wako wote ili wajue jinsi ya kutekeleza kazi zao na kufanikisha shughuli yako

Gawa majukumu:
Kukaribisha wageni
Kupokea zawadi
Kutambulisha ndugu
Kumalizia malipo kwa watoa huduma wako mtu huyu awe unayemuamini, si ajabu mtakua naye katika safari yote ya kuandaa shughuli yako

Wedding theme/Dhana za harusi
Unajua kwamba unaweza kuipa harusi yako dhana Fulani? Hebu angalia mifano:
Classic white wedding
Traditional wedding
Beach wedding
Cocktail wedding
Barbecue